

# UTUKUFU WA MUNGU

Marcus Mtinga  
22.10.2005 Tabata DSM

The musical score consists of four staves of music, each with a treble clef and a key signature of one flat. The music is in common time. The lyrics are written below the notes, corresponding to the vocal parts.

U tu ku fu wa ke Mwe nye zi Mu ngu ni wa mi le - le, U we zo wa

ke u ku u wa ke ha u na mwi - sho, tu si lo we za si - si kwa ke ye -

ye ni ka ma ma - - ji, a ki nyo o sha m ko - no ki la ki tu ki na ku wa shwa

- ri, kwe li Mwe nye zi Mu ngu u we zo wa ko ni wa a ja bu, we

ma fa dhi li za      ko hu ru ma kwe      li ye ye ni Ba      ba,      a me      m pe le ka Ro  
 ho wa ke a me      u fa = nya u      pya,      u      pya u so wa n      chi.      a me  
 i ge u za ba ha      ri yo te sa - sa ni n chi ka      vu,      ma      mbo ni ya a ja      bu.

2. Furahi sana binti Sayuni piga makofi, Mwenyezi Mungu amesikia kilio chako,  
Amewatupa chini wenyenzi na viti vyao, amewakweza wanyonge rehema zake zikawa kwako,  
Kweli Mwenyezi Mungu.....
3. Tumeuona wema wako mwenyezi Mungu, upole wako unatupunguzia uchungu,  
katika maisha yetu unatufunza kuvumilia, magumu yakitusonga watupa moyo tunayabeba,  
Kweli Mwenyezi Mungu.....
4. Matatizo yetu unayajua vema Baba, udhaifu wetu unaujua vema sana tu!  
Sisi peke yetu Baba hatutaweza kufika vema, msaada wako mwema huruma yako utupe hima  
Kweli Mwenyezi Mungu.....
5. Tunayakabidhi maisha yetu moyoni mwako, furaha, dhiki taabu zetu viwe ni vyako,  
Utulinde ututunze kwa nguvu zako tuwe salama, na hii safari yetu kurudi kwako iwe salama,  
Kweli Mwenyezi Mungu....